HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI MHE. PROF MARK MWANDOSYA (MB), WAKATI WA KUKABIDHI KWA BAADHI YA HALASHAURI MAGARI 61 NA SCANNER 56 ZA KUTEKELEZA PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA, TAREHE 1 MACHI, 2010

Ndugu Christopher Sayi, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Wakurugenzi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya,
Wafanyakazi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Ndugu Waandishi wa Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Utangulizi

Ndugu Washiriki Mabibi na Mabwana, ninayo furaha ya pekee kuwa pamoja nanyi katika hadhara hii muhimu, ya kushuhudia moja ya hatua zinazotekelezwa na Serikali katika kuhakikisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekelezwa kikamilifu kufikia malengo yaliyowekwa ya kuboresha huduma za maji nchini na kuboresha maisha ya wananchi. Programu hii inatekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Dira hiyo inalenga kuwapatia huduma ya maji ya kuridhisha wananchi waishio vijijini na mijini ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa Dira hiyo umegawanywa katika vipindi vya muda wa kati na muda mfupi. Katika muda wa kati, Serikali imeridhia Malengo ya Kimataifa ya Milenia ambayo kwa sekta ya maji ni kupunguza kwa **asilimia 50** idadi ya watu wasio na huduma ya maji safi na salama na huduma ya usafi wa mazingira na kuweka mfumo shirikishi wa usimamizi wa rasilimali za maji ifikapo mwaka 2015.

Ili kufikia malengo ya Milenia, Serikali imeandaa MKUKUTA kama mkakati wake wa muda mfupi. Katika mkakati huo, Wizara ya Maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama karibu na makazi yao kwa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma hiyo kutoka **asilimia 53.5** ya mwaka 2004/2005 hadi **65** ya wananchi waishio vijijini na kutoka **asilimia 73** ya mwaka 2004/2005 hadi **90** ya wananchi waishio mijini ifikapo mwaka 2010.

Katika kuhakikisha malengo ya MKUKUTA yanafikiwa, mwezi Desemba 2006, Serikali ilikamilisha maandalizi ya **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji** na utekelezaji wake ukaanza katika mwaka wa fedha 2007/2008. Programu hiyo inatekezwa katika programu ndogo nne: (i) Programu ya usimamizi wa rasilimali za maji; (ii) Programu ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini (iii) Programu ya utoaji wa huduma za majisafi na majitaka mijini; na (iv) Programu ya kuimarisha taasisi za Sekta ya kuzijengea uwezo

Ngazi za utekelezaji

Ndugu Washiriki Mabibi na Mabwana, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekelezwa na Serikali katika ngazi kuu nne ikiwa ni pamoja na ngazi ya Serikali kuu ikishirikisha Wizara yangu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ngazi nyingine ni ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa na ngazi ya nne na ya tano ni kwenye Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa na wilaya na miji midogo na katika Bodi za Maji za mabonde ya maji nchini.

Serikali Kuu ina jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji katika ngazi za chini za utekelezaji na pia kuzijengea uwezo ngazi hizo kwa kuzipatia vifaa, na nyenzo za kufanyia kazi pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi wa taasisi hizo kulingana na na Sera ya Serikali ya kukasimia madaraka na rasilimali katika ngazi za nchini ya utekelezaji. Lengo la Sera hiyo ni kusogeza karibu huduma kwa kuziwezesha taasisi zinazotoa huduma hizo kwa wananchi kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kwa ufanisi.

Kwa upande wa Halamshauri fedha za kutekeleza sekta ya maji zinatumwa wilayani chini ya utaratibu wa kutoa ruzuku za kutekeleza miradi ya maendeleo na kujenga uwezo wa serikali za mitaa *(Local Government Development Grant System – LGDG)*. Vigezo vya kugawa fedha kwa kila Halmashauri viliwekwa kulingana na majadiliano na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Wizara yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Uchumi. Vigezo vya kugawa fedha kwa kila Halmashauri vinazingatia idadi ya watu ambao bado hawajapata huduma ya maji na aina ya teknolojia inayotumika katika miradi ya maji katika kila Wilaya. Vigezo hivyo ni juhudi za makusudi za Serikali kuinua viwango vya huduma ya maji katika Wilaya ambazo huduma hiyo iko chini ili kuleta uwiano wa huduma hiyo katika Wilaya zote nchini.

Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Ngazi za Halmshauri

Ndugu Washiriki Mabibi na Mabwana, utekelezawa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Ngazi za Halmshauri inahusu ujenzi wa miundombinu ya maji vijijini, uhamasishaji wa wananchi kuhusu usafi wa mazingira vijijini, na uimarishaji wa Halmashauri ili kuziwezesha kutekeleza majuku yake kikamilifu. Katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa programu, utekelezaji ulioanza mwaka 2007/2008, **shilingi bilioni 87.4** kutoka kwenye mfuko wa pamoja wa fedha za sekta ya maji (*Water Basket Fund*) zimetumika. Mfuko huo unachangiwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, Serikali ya Ujerumani na Serikali ya Uholanzi. Jumla ya **shilingi bilioni 123.4** zimetumika nje ya mfuko wa pamoja *(earmarked funding)* na zimepelekwa moja kwa moja kutekeleza miradi katika Halmashauri mbalimbali nchini. Fedha hizo zimetoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Serikali za Japan, Ujerumani na Korea ya Kusini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yakiwemo Global Aid Network ya Canada, Water Aid, Concern, Plan Tanzania na Mashirika ya Kidini. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho yamewezesha kiwango cha huduma ya maji vijijini kupanda kutoka asilimia 55.7 mwaka 2006 hadi 61.3 mwezi Deseaba mwaka 2009.

Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo, Halamshauri, taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, madhehebu ya kidini, na wananchi kwa kwa ushirikiano waliotoa katika kufikia mafanikio hayo.

Vifaa na Nyenzo za Kufanyia Kazi

Ndugu Washiriki, kama nilivyodokeza hapo awali, jukumu mojawapo muhimu la Serikali ni kuzijengea uwezo taasisi za utekelezaji katika ngazi za nchini ikiwa ni pamoja na Halmashauri, Mamlaka za Maji Mijini na Boda za Maji za Mabonde. Kati ya mwezi Novemba 2009 na Januari 2010, vitendea kazi vifuatavyo viligawiwa kwa watekelezaji hao:

(i) Pikipiki 252 na P*rinter* 111 kwa Halmashauri;

(ii) Pikipiki 120 kwa Mamlaka za Maji Mijini

(iii) Pikipiki 35, *River gauging boat* na *Engine* zake (25), *Life jackets* (90) na *Wading suits* (90), kwa Boda za maji za mabonde; na

(iv) Magari 21 kwa Sekretarieti za Mikoa.

Ndugu Washiriki, katika hafla ya leo ni nitawakabidhi Wakurugenzi wa Halmashauri 61 magari tuliyopokea hadi sasa kati ya magari tunayotarajia kupokea kutosheleza Halmashauri zote nchini. Pia nitakabidhi mashine kudurufia (Scanner) 56 kwa Halmashauri zile ambazo zilizokwishapokea *printer*. Huu ni mwendelezo katika kuhakikisha halamashauri, mamlaka za maji mijini na Bodi za Maji za Mabonde zinawezesha vya kutosha ili ziweze kutekeleza majuku yao kikamilifi katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

Halmashauri 61 zitakazopata magari hivi leo ni kama ifuatavyo:

(i) **Mwanza:** Halmashauri za Geita, Magu, Jiji la Mwanza, Sengerema, Kwimba, Misungwi, Ukerewe;

(ii) **Shinyanga:** Halmashauri za Bariadi, Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, Maswa, Kahama, Meatu, Kishapu, Bukombe;

(iii) **Kagera:** Halmashauri za Biharamulo, Manispaa ya Bukoba, Bukoba, Karagwe, Misenye, Muleba, Chato, Ngara;

(iv) **Mara:** Halmashauri za Bunda, Manispaa ya Musoma, Musoma, Serengeti, Tarime, Rorya;

(v) **Tabora:** Halmashauri za Igunga, Sikonge, Nzega, Tabora, Urambo, Tabora/Uyui;

Rukwa: Halmashauri za Mji wa Mpanda, Mpanda, Nkasi, Sumbawanga, Manispaa ya Sumbawanga;

(vi) **Kigoma:** Halmashauri za Kasulu, Kibondo, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kigoma;

(vii) **Manyara:** Halmashauri za Hanang', Mbulu, Babati, Mji wa Babati, Kiteto, Simanjiro;

(viii) **Mtwara:** Halmashauri ya Nanyumbu;

(ix) **Mbeya:** Halmashauri za Ileje, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Rungwe, Chunya, Kyela, Mbozi, Mbarali;

(x) **Arusha:** Halmashauri ya Ngorongoro; na

(xi) **Lindi:** Halmashauri ya Liwale.

Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, ningependa kuchukua fursa kuwasihi myatunze magari haya na kuyatumia kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuboresha utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na siyo kwa ajili ya shughuli nyingine au za binafsi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA